
HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE



Simu: 028-2227148
Fax: 028-2227140
E-mail ded.karagwe@kagera.go.tz
ded@karagwedc.go.tz

S. L. P. 20,
KARAGWE

Kumb.Na.KGR/HWK/T.10/1/VOL.XVI/111

23/03/2018

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kupitia Kibali cha Ajira kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Utumishi chenye Kumb. Na. CFC.26/205/01/"FF"/91 kilichotolewa tarehe 22 Agosti, 2017 anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kuajiriwa katika kada ya Mtendaji wa Kijiji III:-

1. Mtendaji wa Kijiji III (Village Executive) Nafasi ishirini na sita (26)

A. SIFA ZA WAOMBAJI

- Waombaji wawe na Elimu ya Kidato cha Nne au cha sita na mafunzo ya Astashahada au cheti katika moja ya fani zifutazo:-
 - Utawala
 - Sheria
 - Elimu ya Jamii
 - Usimamizi wa Fedha
 - Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali .

B. KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI III

- Kuratibu na kusimamia upangaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao
- Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Kijiji
- Kusimamia, kukusanya kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Vijiji
- Katibu wa Mikutano ya Halmashauri ya Kijiji
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Vijiji
- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi

